

**SALAMU ZA RAMBIRAMBI KUTOKA**  
**NEW ENGLAND UMOJA FOUNDATION.INC**



**UMOJA WA WATANZANIA WAISHIO "NEW ENGLAND STATES"**  
(Massachusetts, Connecticut, Rhode Island, Maine, New Hampshire, Vermont, New Jersey)

NCHINI MAREKANI, TUNAUNGANA NA WATANZANIA POPOTE WALIPO DUNIANI KWA KUTUMA SALAMU ZA RAMBIRAMBI KWA WANANCHI WENZETU, HASA NDUGU, JAMAA NA MARAFIKI WALIOJERUHIWA, TUNAOMBOLEZA KWA WALE WOTE WALIOPOTEZA MAISHA YAO KWENYE MILIPUKO YA MABOMU KATIKA KAMBI YA JESHI MAENEO YA GONGO LA MBOTO, DAR-ES-SALAAM.

TUNAMUOMBA MWENYEZI MUNGU AWAPUMZISHE MAREHEMU WOTE MAHALI PEMA PEPONI. TUTAZIDI KUWAOMBEA WALE WOTE WALIOJERUHIWA NA KUWATAKIA KILA LA KHERI WAPONE HARAKA.

WATANZANIA WOTE TUISHIO PEMBE HII YA MASHARIKI MWA MAREKANI TUNACHUKUA NAFASI HII KUWAPONGEZA WANANCHI WENZETU MLIKO NYUMBANI, VYOMBO VWA WATU BINAFSI, TAASISI NA MASHIRIKA MBALIMBALI, NA PIA VYOMBO VYA SERIKALI, KWA UPENDO NA MOYO WA KUJITOLEA MLIUONYESHA KATIKA KUWAHUDUMIA MAJERUHI, KUWAFARIJI WALE WOTE WALIOATHIRIKA NA WASIOKUWA NA MAKAZI YA KUISHI, WALIOPOTELEWA NA NDUGU, JAMAA NA MARAFIKI, KINAMAMA NA WATOTO, NA HASA KATIKA KUSHIRIKI KWENYE MAZISHI YA WENZETU WALIOPEZA MAISHA YAO.

MUNGU IBARIKI TANZANIA NA WATU WAKE.  
New England Umoja Foundation, Inc. [www.newenglandumoja.net](http://www.newenglandumoja.net)